

## Kunyunyuzia maji

Iwapo mvua katika sehemu yako haitoshelezi maharagwe haya, basi waweza kunyunyuzia mimea maji baada ya matumba kufanyika. Hii yaweza kusaidia kuongeza mazao.

## Magonjwa na wadudu

Magonjwa ya kawaida ya maharagwe huyapata maraharagwe haya ya kutambaa. Ni vyema kutumia mbegu zilizothibitishwa na vile vile kutumia madawa yafaa.

## Uharibifu wa ndege

Ndege kwa kawaida huharibu maharagwe yanayotambaa. Huwa wanakula maharagwe changa, maua na matumba changa.

Kuwafukuza na kuwatisha husaidia kupunguza uharibifu wao.

## Kuvuna

- a) Kuvuna kufanywe wakati ufaao kulingana na matumizi.
  - Vuna wakati matumba imejaa mbegu ikiwa matumizi ni ya mboga,
- b) (b) Kwa matumizi ya maharagwe yaliyo kauka yanafaa kuvunwa punde yanapo kauka. Walakini, matumba hukauka nyakati tofauti.

## Uhifadhi

Maharagwe yaliyokaushwa na kutenganisha na uchafu, huwekwa dawa na kuhifadhiwa kwenye ghala kwa matumizi.



### Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

#### Watayarishi:

Muthamia, J. Micheni, A. na Karanja, D

#### Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

#### Mkuu wa Kituo,

Kari-EMbu, S.L.P. 27 Embu


Simu: 068 20116/ 20873

Nukulishi: 06830064

Baruapepe: kariembu@salpha.co.ke

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 30 /2008

**Usaidizi wa kifedha na wa kitaaluma wa ECABREN na PABRA umefurahiwa sana**



# Ukuzaji wa maharagwe yanayotambaa ili kupata mazao ya juu



## Utangulizi

Maharagwe yanayotambaa ni maharagwe yenye uwezo wa kutambaa hadi urefu wa mita 4. Yana mazao ya juu na hukomaa katika msimu mmoja tu. Yanahitaji vifaa vya kuyashikilia na wafanyikazi ambao wamefunzwa jinsi ya kutengeneza vifaa hivyo.



## Kwa nini tukuze maharagwe yanayotambaa?

- Mazao yake yanaweza kuzidi tani 5 kwa kila eka.
- Yanaongeza nitrojeni kwa mchanga na pia hutengeneza tani 17 hadi 25 za majani kwa kila eka.
- Yana faida ya juu kuliko maharagwe ya kawaida.

## Aina za maharagwe yanayotambaa

Kuna aina tatu za maharagwe yanayotambaa miongoni mwa wakulima wa Kenya.

AINA ZA MAHARAGWE YANAYOTAMBAA			
Kielelezo	MAC 13	MAC 34	MAC 64
Kielezo Aina Aina ya Rose	Aina ya Rose coco, yenye weupe zaidi	Aina ya Rose coco, yenye weupe zaidi	Aina ya Rose coco, yenye weupe zaidi
Ukubwa wa mbegu	Kubwa	Kubwa	Kubwa
Maumbile ya mbegu	Figo	Kama kisu	Kama kisu
Wakati wa kukomaa	Siku 95	Siku 105	Siku 120
Uwezo wa mazao	Tani 4 hadi 5	Tani 4 hadi 5	Tani 4 hadi 5

## Jinsi ya kukuza maharagwe yanayotambaa

### Utayarishaji ardhi

Unaweza kulima ardhi yako kwa mkono, kutumia wanyama au tingatinga ili kuutayarisha mchanga na kuua kwekwe.

### Nafasi

Tengeneza mashimo yalipo na nafasi ya sentimita 75 kwa kila sentimita 30 na upande mbegu mbili (2) kwa kila shimo.

### Mbolea

Maharagwe yanayotambaa huhitaji kiasi kingi cha madini. Tia mbolea ya kimo cha mikono uliyojaa katika kila shimo na uchanganye vizuri na mchanga.

### Mbolea ya kuimarisha mazao

Tumia DAP, 20:20:0, au 17:17:17 kiwango cha gramu 5 (kijiko cha chai) kwa kila shimo na uchanganye vizuri na mchanga kabla ya kupanda mbegu.

## Kushikiliwa

Maharagwe yanayotambaa huitaji kushikiliwa ili kusaidia kuupa mmea hewa ifaayo na kupunguza kuwepo kwa maradhi.

- Mazao hutegemea urefu kwa hivyo vishikilio vinafaa kuwa zaidi ya urefu wa mita 3.

Mbinu za kushikilia ni:

- Vijiti kwa kila mmea.
- Vikingi na waya au uzi.



Kijiti kwa kila mmea



Vifaa vya kushikilia ni kama waya, uzi na nguzo